NIPASHE UK 9

# LITA yatakiwa kutoa elimu ya mifugo

Na Beatrice Shayo

KATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia mifugo, Tixon Nzunda, ameutaka Wakala wa Elimu ya Mafunzo ya Mifugo nchini (LITA) kuhakikisha inatoa elimu bora ya mifugo ndani na nje ya nchi.

Nzunda aliyasema hayo jijini Dodoma wakati akifungua kikao cha tisa cha Baraza Kuu la Wafanyakazi la LITA na kuwataka kuwa chanzo cha kuwashauri wafugaji na kutoa maarifa kwa wadau wa sekta ya mifugo ili sekta hiyo iweze kuimarika na kuwa ya kisasa zaidi.

Alisema wakufunzi wa LITA wanatakiwa kuwa chanzo cha kuandaa majarida mbalimbali yakiwamo vitabu vya ufugaji na kupatikana kwa maarifa mapya yanayotokana na utafiti zinazofanywa na wakufunzi hao.

Aidha, alisema wajibu wake ni kuwa karibu na umma kwa kutoa huduma bora ikiwamo ya wanafunzi wanaohitimu kuwa bora na wanaoheshimika, kutambulika wenye maarifa, waaminifu na kuandaliwa vizuri kwenda kusaidia sekta binafsi.

Awali, Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Wafanyakazi la LITA, Dk. Pius Mwambene, alisema baraza hilo limeendelea kuimarisha uhusiano na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha inaboresha miundombinu ya kufundishia.

Dk. Mwambene alisema kwa sasa wakala huo unakaribia kukamilisha makubaliano ya ujenzi wa kampasi ya LITA mkoani Songwe ikiwa ni jitahada za kuongeza wigo wa elimu ya mifugo katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema katika kuhakikisha wafugaji wanapata mwongozo wa ufugaji bora imeanisha utaratibu wa kuwashikiza wanafunzi wa hatua ya nne kwa wafugaji katika maeneo yao wakati wa likizo ili kuanza kujenga uzoefu ujasiri wa kuwahudumia wafugaji mapema.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Angello Mwilawa, alisema wataendelea kusimamia maadili na weledi kwa wafanyakazi na kuongeza ushirikishwaji ili kuwapo na matokeo makubwa yenye maslahi mapana yatakayoleta tija.

Dk. Mwilawa alisema nguvu zaidi zitaelekezwa kwenye maeneo ambayo yatagusa jamii na maelekezo yote yatafanyiwa kazi ili kuongeza ufanisi.

Baadhi ya wajumbe wa baraza katika kikao hicho, wametoa mapendekezo kadhaa ya kuboresha utendaji kazi pamoja na mazingira ya wafanyakazi ili waweze kufanya kazi kwa morali na kufikia malengo.

Scanned with CamScanner

# Kahawa, samaki vyaongoza mauzo soko la Ulaya

Na Evance Ng'ingo

KAHAWA kutoka Tanzania imeongoza kuuzwa katika soko la Ulaya (EU) kwa mwaka jana na kuingizia nchi takribani Euro milioni 68.

Hata hivyo, zao hilo kama Tanzania ikijipanga vyema imeelezwa kwamba linaweza kuuzwa hadi kufikia Euro milioni 168.

Hayo yamebainishwa kwenye ripoti iliyozinduliwa jana inayoonesha mchango wa uwekezaji ya EU kwa Tanzania na namna umoja huo unavyochangia maendeleo ya viwanda na maendeleo kwa ujumla.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo mazao yanayofuatia ni samaki wabichi na kokoa, mazao ambayo pia yameelezwa kwamba yana nafasi kubwa ya kuuzwa zaidi ya kiwango cha sasa Ulaya.

Mazao mengine yaliyofanya vizuri kwenye soko la Ulaya ni ufuta, mbogamboga zinazolimwa kitaalamu (unrooted cuttings), parachichi na korosho.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Tanzania imeuza bidhaa zenye thamani ya Euro milioni 456 Ulaya huku nchi za Ulaya zikiingiza nchini bidhaa zenye thamani ya Euro milioni 856 katika kipindi hichohicho.

Bidhaa kubwa kutoka EU inayoingia nchini ni dawa za binadamu. Nyingine ni matrekta, magari, dawa za kuua wadudu, ngano, vifaa vya maabara, vipuri vya magari na kadhalika.

Ripoti hiyo ilizinduliwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula kwa niaba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Akizungumza baada ya uzinduzi wa ripoti hiyo, Waziri Mulamula alibainisha kuwa mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyowekwa na Rais Samia Suluhu Hassan yamechagiza kuendelea kuwepo uwekezaji mkubwa wa kampuni za EU hapa nchini.

"Hii ripoti imetuonesha matokeo ya hatua nzuri ambazo tumekuwa tunazichukua kama nchi katika kuvutia uwekezaji na pia inatuonesha wapi hasa tunatakiwa kuongeza nguvu zaidi katika kuvutia uwekezaji," alisema.

Alisema kampuni takribani 100 za Ulaya zimewekeza nchini na kusababisha ajira 151,000 na kwamba asilimia 98 ya walioajiriwa kwenye kampuni hizo ni Watanzania, asilimia 38 wakiwa wanawake.

Mkurugenzi Mtendaji wa European Union Business Group (EUBG), iliyoshiriki kuandaa ripoti hiyo, Cikay Richards alibainisha kuwa kampuni za EU zimekuwa wawekezaji wakubwa nchini hususani katika sekta za kilimo na utalii.

Balozi wa EU nchini, Manfredo Fanti alisema ripoti hiyo mbali na kuonesha namna kampuni za EU zilivyowekeza nchini pia inaonesha fursa nyingi zaidi za kibiashara zilizopo Tanzania na kwa kiasi gani kampuni za nje zinaweza kuja kuwekeza.

Alisema mbali na kufanya biashara, EU imekuwa pia ikisaidia kuwainua wajasiriamali nchini kupitia benki yake ya uwekezaji (European Investment Bank) inayokopesha benki za Tanzania ili nazo zifikishe mikopo kwa wajasiriamali wadogo.

Alisema katika kuhakikisha Tanzania inazidi kunufaika na biashara kwa nchi za EU, umoja huo umeondoa kodi kwa bidhaa kutoka Tanzania.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, David Kihenzile aliutaka EU kuongeza uwekezaji zaidi katika kilimo, mifugo na utalii.

Akitoa mfano, alisema kupitia sekta ya mifugo Tanzania inatakiwa iwe inauza Ulaya bidhaa zitokanazo na mifugo kama ngozi na nyama.

Scanned with CamScanner

kuwahamasisha wanachama wenye nia wagombee kwa uadilifu ili kuendelea kukijenga na kukiimarisha Chama .

Katika mkutano huo, Mbunge huyo aligawa vyeti kwa wanachama na viongozi mbalimbali wa kata hiyo waliofanya kazi za Chama vizuri akiwemo Diwani wa Viti Maalumu Kibaha, Lidya Mgaya.

Alikabidhi viti 25 vya plastiki vyenye thamani ya sh. 450,000 katika mradi wa vijana wa kata hiyo.



Uhuru, uk 9.

# Diwani aahidi kuwatafutia ufumbuzi wafanyabiashara wa ng'ombe, mbuzi

**Na CHRISTOPHER LISSA**

DIWANI wa Kata ya Pugu Stesheni, Shabani Mussa, atashiriki kikamilifu katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyabiashara wa ng'ombe na mbuzi wa kata hiyo.

Mussa aliyasema hayo juzi alipokutana na wafanyabiashara hao ambao walimweleza kwamba, miongoni mwa changamoto zinazowakabili ni ada kubwa ya usajili wanayotozwa kiasi cha sh. 70,000 kwa mwaka.

Alisema anatambua changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyabiashara katika mnada wa Pugu, akaahidi kuwa mstari wa mbele kushiriki kuzitatua ikiwemo kuzifikisha katika mamlaka husika.

Kwa mujibu wa Mussa, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, ni sikivu, hivyo aliwataka wafanyabiashara katika mnada huo, kuwa watulivu wakati kero zao zikitafutiwa ufumbuzi.

"Kwa nafasi yangu kama diwani, nazipokea changamoto hizi, ninaahidi kuzifikisha katika mamlaka husika ili kujenga ushirikiano mzuri kati ya wafanyabiashara na serikali," alisema.

Katika hatua nyingine, diwani huyo aliwahimiza wafanyabiashara hao kushiriki kikamilifu katika sensa ya watu na makazi ili iwe rahisi kwa Serikali kuwatambua na kuwafikishia fursa za maendeleo.

Pia, aliwataka wafanyabiashara hao kusajiliwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Pugu Stesheni kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo lao la kibiashara na mitaa yote mitatu ya Kata hiyo.

"Kwa kuwa tumekubaliana hapa katika kikao hiki, suala la kujisajili ni muhimu ili kuimarisha ulinzi katika kata yetu. Pia, lazima tutambuane ni wafanyabiashara wangapi wa mbuzi na ng'ombe tulionao katika kata yetu.

"Tusipokuwa na mpango mzuri wa kutambuana wanaweza kuja watu wakatumia fursa hiyo kufanya vitendo vya kihalifu ila tukitambuana itarahisisha utendaji kazi katika shughuli zetu za kila siku," alisema..

Alisema wafanyabiashara katika mnada huo, watasajiliwa na kupewa vitambulisho maalumu, hivyo aliwahimiza kushiriki muda wa kujisajili utakapowadia ambapo uongozi utaweka utaratibu mzuri katika ngazi ya kata utakaorahisisha usajili huo.

Awali, wafanyabiashara hao, walimweleza diwani huyo kuwa, moja ya kero kubwa ni ada ya usajili wanayotozwa ya sh. 70,000

"Tunakuomba tusaidie kulifikisha hili katika mamlaka husika kwa sababu, kiasi hiki ni kikubwa na hakiendani na vipato vyetu," alisema mfanyabiashara wa mnada huo, Odunga Omo.

Scanned with CamScanner